JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

# MAREKEBISHO YA MWALIKO WA MAOMBI MAPYA NA UPANDISHAJI DARAJA WA LESENI ZA MAUDHUI YA REDIO ZA FM ULIOTOLEWA TAREHE 7 NOVEMBA 2024

Mwaliko wa Maombi mapya na Upandishaji Daraja wa Leseni za Maudhui ya Redio za FM uliotolewa tarehe 7 Novemba 2024 na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) unarekebishwa katika maeneo yafuatayo:

**A. Maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya Maombi Mapya, Upandishaji wa Daraja au Kuongeza Maeneo ya Huduma za maudhui ya Redio za FM.**

| Mkoa | Eneo la Huduma | Idadi ya Masafa ya FM yaliyopo |
|---|---|---|
| Morogoro | Malinyi | 1 |

**B. Maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya Maombi ya Upandishaji wa Daraja au Kuongeza Maeneo ya Huduma za maudhui ya Redio za FM.**

| Mkoa | Eneo la Huduma | Idadi ya Masafa yaliyopo ya FM |
|---|---|---|
| Morogoro | Morogoro | 4 |

1. Waombaji wanatakiwa kuzingatia **Mwongozo** wa uwasilishaji wa maombi unaopatikana katika tovuti ya TCRA: **www.tcra.go.tz**

2. Maombi yote ya utoaji wa huduma tajwa hapo juu yawasilishwe kwa kupitia mfumo wa maombi ya leseni wa TCRA uitwao **Tanzanite Portal** kupitia kiunganishi kifuatacho: **https://tanzanite.tcra.go.tz/index.htm** kabla ama ifikapo tarehe **7 Disemba, 2024.**

3. Tafadhali zingatia kwamba, endapo waombaji katika eneo fulani la huduma wako wengi zaidi ya kiasi cha Masafa yaliyoainishwa katika eneo hilo, **TCRA itaweka Masafa ya eneo husika katika mchakato wa ushindani yaani Zabuni/Mnada**.

4. Waombaji watakaoingia kwenye **mchakato wa ushindani wa zabuni au mnada watajulishwa ili waweze kuwasilisha zabuni zao katika bahasha iliyofungwa ambayo itafunguliwa mbele ya wazabuni wote.**

Imetolewa tarehe **15 Novemba, 2024**

Dkt. Jabiri K. Bakari

**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz